

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

638

VIELELEZO NA TEKNOLOJIA

Muda: Saa 3

Jumatatu, 11 Mei 2015 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B.
2. Jibu maswali **yote** kutoka katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu B.
3. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Eleza njia kuu zisizopungua nne za upatikanaji wa vielelezo na teknolojia kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.
2. Toa sababu nne zinazofanya kitabu cha kiada kipewe kipaumbele kuliko machapisho mengine.
3. Eleza kwa kifupi faida nne za kutumia nyimbo wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.
4. Eleza kwa kifupi kwa nini ni muhimu kufanyia majaribio zana za kufundishia na kujifunzia kabla ya kuzitumia darasani. Toa hoja nne.
5. Chambua kwa kifupi mambo manne yanayoweza kusababisha uelewa wa wanafunzi kuwa chini au juu ya umri wao.
6. Eleza kwa kifupi umuhimu wa vielelezo kwa mwalimu wakati wa kufundisha na kujifunza (Toa hoja nne).
7. Elezea changamoto nne zinazoweza kujitokeza katika matumizi ya vielelezo na teknolojia masikizi-maono.
8. Eleza kwa kifupi mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa katika upatikanaji wa makunzi kwa ajili ya kutengenezea zana za kufundishia na kujifunzia.
9. kwa nini matumizi ya vielelezo na teknolojia asilia humjengea mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu. Toa sababu nne.
10. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia.
(b) Fafanua hatua tatu zinazotakiwa kufuatwa kabla ya kufaragua na kutengenezea zana za kufundishia.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (04)** kutoka katika sehemu hii.

11. “Utunzaji wa zana za kufundishia na kujifunzia ni ketendo muhimu kwa walimu shuleni.” Thibitisha usemi huu kwa kutoa hoja tano.
12. Fafanua mambo matano yanayoweza kusababisha tendo la kufaragua zana kuchukua nafasi ya kwanza kuliko kubuni na kutengeneza.
13. Elezea kazi tano za vielelezo na teknolojia masikizi-maono katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.
14. Kwa nini ni muhimu kwa mwalimu kujifunza mbinu za kufaragua vielelezo kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia? Toa hoja tano.
15. Kanusha kauli kwamba “utumiaji wa vielelezo na teknolojia hauna manufaa zaidi ya kupotezea wanafunzi muda wao wa kujifunza” (Toa hoja tano).
16. Eleza njia tano zinazoweza kutumika katika kuhifadhi vielelezo na teknolojia ili viweze kudumu kwa muda mrefu.
17. Kwa kutumia mifano, thibitisha umuhimu wa kompyuta kama moja ya vielelezo na teknolojia kisasa kinachoweza kutumika katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.
18. Eleza hatua kwa hatua jinsi mwalimu anavyoweza kutengeneza ramani ya Afrika ardhini kwa kutumia makunzi anuai.